

Utiifu Uliotiwa Mafuta

Sura ya 9

Somo la Kusikiza: Uchunguzi wa Agano la Kale Somo la 35



Shabaha: Kuelewa tofauti muhimu kati ya maisha ya Sauli na maisha ya Daudi.



moyo.”

“Lakini BWANA akamwambia Samueli, usimtaame uso wake, wala urefu wa kimo chake; kwa maana mimi nimemkataa. BWANA haangalii kama binadamu aangaliavyo; maana wanadamu huitazama sura ya nje, bali BWANA huutazama

— 1 Samueli 16:7

Kutotii kwa Sauli kulisababisha Bwana amtupilie mbali kutoka kwa uwepo wake na kuondoa Roho wake Mtakatifu kutoka juu yake. Hilo lilipofanyika, maisha ya Sauli yalirudi kuwa maelezo yanayotembea ya kile tunaita katika desturi yetu kuporomoka kwa utu.

Maisha ya Daudi yalikuwa kinyume kabisa na maisha ya Sauli. Tabia kuu katika maisha ya Daudi ilikuwa kutii – alikuwa mtu wa kufuata moyo wa Mungu ambaye angefanya yote atakayo Mungu. Mahali ambapo maisha ya Sauli yalikuwa yanaporomoka kwa sababu alikuwa amejitalaki kutoka kwa Mungu, Mungu alikuwa analeta kila kitu pamoja katika maisha ya Daudi kwa sababu Daudi alikuwa amelenga zaidi utiifu na Sauli alikuwa amelenga kutotii.

Daudi alikuwa mchungaji, mwana muziki, mwanajeshi, kiongozi, na rafiki. La muhimu kuliko yote, anaelezewa kuwa mtu aliyefuatilia moyo wa Mungu.



1. Ukweli au uongo? Mungu anahusika tu na vile tunavyofanana sawa na vile anavyohusika na usafi wa mioyo yetu.
2. Ukweli au uongo? Daudi alifanyika mfalme mara tu Samueli alipomtia mafuta.
3. Ukweli uongo? Mungu alichukuwa miaka akimuandaa Daudi kuwa mfalme.

Ikiwa hujaambiwa lingine la kufanya, basi, chagua jibu moja tu kwa kila swali lifuatalo.

4. Gani kati ya maneno yafuatayo yanamuelezea Daudi? (*Chagua yote yanayotumika*)
 - a. Wa kiungu
 - b. Dhaifu
 - c. Wa kimuziki
 - d. Mtiifu
 - e. Mwenye nguvu na mjasiri
 - f. Mwenye umbo nzuri
 - g. Mwenye nia mbili
 - h. Mwoga
 - i. Shujaa

5. Gani kati ya maneno yafuatayo yanayomwelezea Sauli? (*Chagua yote yanayotumika*)
 - a. Wa kiungu
 - b. Mwenye wasi wasi mkubwa
 - c. Mwaminifu
 - d. Mwenye nguvu
 - e. Dhaifu
 - f. Mwenye wivu
 - g. Asiye mtiifu
 - h. Mwanamziki
 - i. Wa vita

6. Kwa nini Daudi alipigana na Goliathi?
 - a. Alidhania yeye ni mwenye nguvu kuliko Goliathi
 - b. Alidhania Goliathi atajisalimisha
 - c. Alitaka apandishwe cheo
 - d. Alighadhabishwa kuwa Mungu na watu wake walikuwa wanatukanwa

7. Watu wa Daudi walijihisi vipi kuhusu Daudi?
 - a. Walikuwa waaminifu
 - b. Walimchukia
 - c. Walimpenda Sauli kwa uafadhali
 - d. Walimwogopa

8. Uhusiano wa Daudi na Yonathani unaelezewa kuwa vipi?
 - a. Usio na maadili
 - b. Kama mshindani
 - c. Kama urafiki wakupendeza
 - d. Kama baba na mama

9. Kwa nini Daudi alikuwa mkimbizi kutoka kwa mfalme Sauli?
- Yonathani alimuuliza babake amuue Daudi
 - Daudi alimtendea Sauli dhambi na ikabidi akimbie
 - Sauli alitaka kumfanya Daudi kuwa mfalme lakini Daudi hakutaka kuwa.
 - Sauli alikuwa na wivu wa kichaa eti kwa sababu Mungu alikuwa amemchaguwa Daudi
10. Daudi aliandika nini alipokuwa mkimbizi?
- Kitabu cha Ruthu
 - Maalezo ya maisha yake
 - Sehemu kubwa ya Zaburi
 - Barua kwa wafuasi wa Sauli
11. Mungu alitumia nini kumwandaa Daudi kuwa mfalme? (*Chagua yote yanayokubaliana*)
- Alikuwa ndugu mdogo, wa mwisho kwa wandugu wanane
 - Alikuwa na kazi ya kuudhi ya kuchunga kondoo
 - Aliulizwa kuongoza Jeshi la kushinda jitu
 - Alipata kazi ya kucheza kinanda katika ikulu la mfalme
12. Mungu alimwahidi Daudi nini?
- Kumfanya mfalme wa sehemu yote ya Asia
 - Kuimarisha ufalme wake milele
 - Kumuacha Daudi ajenge hekalu kwa ajili ya Mungu
 - Kukatiza kizazi chake kabisa



Wakati Mungu anaangalia moyo wako, unafikiria anaona nini? Je, kunazo sehemu fulani ambazo umemnyima Mungu? Ni “majitu gani” – hali zisizo wezekana zinazotaribu imani yako – ambazo unakumbana nazo? Katika njia gani unaweza toa moyo wako zaidi kwa Mungu?



Uliza Mungu akupe moyo kama wa Daudi. Mushukru kuwa amekutafuta umjue na umpende.



KUZAMA ZAIDI

1. Tofautisha chenye watu waliona walipomwalia Sauli na chenye Mungu aliona kupitia kwa macho ya Samueli alipomwalia Daudi (1Samueli 16:7). Linganisha haya na kile Yakobo anaita dhambi ya kuonyesha upendeleo, ubaguzi, au kulingana na Tafsiri ya Mfalme Yakobo, dhambi ya kuheshimu watu. (Yakobo 2:1-9) _____

2. Mungu aliona nini alipoangalia moyo wa Daudi? _____

3. Je, wewe huweka uthamani wa watu kwa kuegemea namna wanavyofanana nje au kwa kile unaamini kiko mioyoni mwao? Eleza. _____

4. Pangilia vifaa vya kazi na mtindo wa kipawa cha uongozi wa Daudi vilivyo muhitimisha kuwa mfalme bora zaidi ambaye Israeli iliwahi kuwa naye. _____

5. Wakati Daudi alimpiga Goliathi, nini kilicho mchochea, na ujasiri wake ulikuwa juu na nini kwamba kijana mdogo anaweza kuuja jitu la futi 9? _____

6. Maandiko mengi ya Daudi yanapatikana wapi? Yanatuelezea nini kuhusu Daudi alikuwa nini/nani? _____

7. Unapotafakari kubomoka kwa utu wa Sauli na kujengwa kwa utu na maisha ya Daudi, Kwa nini Sauli alimchukia Daudi sana, na inatwambia nini kuhusu tabia ya Daudi alipokataa kumuua Sauli? _____
